

### **SEHEMU YA A: FASIH SIMULIZI (LAZIMA)**

1. (a) Tofautisha kati ya methali na misemo. (Alama 2)
- b) Toa mifano miwili miwili ya methali zinazozingatia tamathali zifuatazo:
  - i) Balagha (Alama 2)
  - ii) Takrir (Alama 2)
  - iii) Ukinzano (Alama 2)
- c) (i) Fafanua vijipera vifuatavyo vyta mazungumzo
  1. Malumbano ya utani (Alama 2)
  2. Soga (Alama 2)
  3. Ulumbi (Alama 2)
- (ii) Taja sifa zozote tatu za soga (Alama 3)
- (iii) Fafanua umuhimu wa soga. (Alama 3)

### **SEHEMU YA B: RIWAYA YA UTENGANO - S.A MOHAMED**

2. Vizuri sana! Kwa sababu damu nzito kuliko maji.
  - (i) Eleza muktadha wa dondo hili. (Alama 4)
  - (ii) Walinganue wahusika wanaorejelewa katika nukuu hii. (Alama 8)
  - (iii) Mwandishi wa riwaya ya Utengano ananuia kuanzisha jamii mpya inayozingatia uadilifu. Thibitisha kwa kutolea mifano yoyote minne. (Alama 8)

### **SEHEMU YA C: TAMTHILIA YA MSTAHIKI MEYA- TIMOTHY AREGE**

3. "Meya Sosi alijua fika kuzichukua hatua za kuhifadhi na kuendeleza utawala wake." Fafanua ukweli wa rai hii kwa kurejelea tamthilia. (Alama 20)

**AU**

4. "Gharama za maisha zinazidi kupanda na mahitaji nayo yanazidi kuongezeka ilhali mshahara haupandi..."
- (a) Tambua muktadha wa dondo hili. (Alama 4)
- (b) Ni mbinu gani za uandishi zilizotumika katika dondo hili? (Alama 2)
- (c) Tofautisha sifa za wahusika wanaopatikana katika dondo hili. (Alama 10)

(d) Fafanua maudhui makuu katika dondo hili na uthibitishe kwa mifano zaidi kutoka kwenye tamthilia. (Alama4)

**SEHEMU YA D: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE-ken walibora na said a. mohamed (wahariri).**

5. “Nashangaa vile kwetu tunavyowaabudu watu hao wasiotujali.”

- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
- b) Fafanua hulka za msemeawa. (alama 6)
- c) Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)

**SEHEMU YA E:USHAIRI**

6. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

**WIMBO WA UNYAGO.**

Ishi kijana ishi, ishi maisha yako.

Wazee waliishi yao

Sasa yamebaki kwako.

Ukabila ni utumwa

Olewa msichana olewa

Olewa chaguo lake

Hiari ni haki asilia

Achaguaye embe bichi

Ajua lini litaiva.

Chunga lugha ya ulaghai:  
 Usikubali kuitwa kipenzi  
 Hiyo ki ni ki ya kitoto;  
 Asifuye macho yako  
 Ataka kuyafumba;  
 Asifuye miguu yako  
 Ataka usitembee;  
 Asifuye meno yako  
 Ataka ucheke kijinga.

Akuandikiaye barua ndefu  
 Ashindwa kusema ukweli;  
 Na kadi maneno ya wengine.  
 Akupigiaye simu kila siku  
 Hana la kusema bali haloo;  
 Asemaye mumeo hafai  
 Nyumbani kwake pia hafai  
 Mbwa aliwekwa utumwani  
 Kwa kifupa kiso mnofu.

Ee mama mwenye rutuba  
 Zaa, zaa kwa mpangilio,  
 Si kufyatua matofali.  
 Zaa ukichunga afya yako.  
 Tawi lenye matawi mengi  
 Huvunjwa na upopo wa tufani.  
 Kumbuka  
 Kuku aliwekwa utumwani  
 Kwa wingi wa vifaranga vyake  
 Ashindwa kujenga kiota.

### **Maswali**

- (a) (i) Shairi hili ni la aina gani? (alama1)  
(ii) Thibitisha jibu lako kwa kutoa sababu zozote mbili. (alama1)
- (b) Jadili maudhui yoyote matatu ambayo mshairi ameyarejelea katika shairi hili. (alama6)
- (c) Taja tamathali ya usemi ilyotawala katika shairi zima na uonyeshe mifano mitatu ya jinsi iliyotumika. (alama4)
- (d) Toa mifano yoyote miwili ya matumizi ya mishata. (alama2)
- (e) Mistari ifuatayo ina maana gani?  
(i) Achaguaye embe bichi  
Ajua lini litaiva.  
(ii) Tawi lenye matawi mengi  
Huvunjwa na upopo watufani.
- (f) Thibitisha kuwa kichwa ‘Wimbo wa Unyago’ kinaafikiana na yaliyomo kwenye shairi hili. (alama 2)

**AU**

### **7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata**

Utendewapo uovu, wa kupituka kivango,  
Moyo siutie chevu, ukautapisha pyongo,  
Na kujipa maumivu, ya fikra na maungo,  
Kipitacho kipe chongo, kitendo hakina kovo.

Lingawa na maonevu, simbulizi na matanga,  
Au la kitenzwa nguvu, hizaya na masimango,  
U singie ulemavu, moyo kuupa kisongo,  
Kipitacho kipe, chongo, kitendo hakina kovu.

Kitendo hakina kovu, sijitie, songosongo,  
 Mcha Mungu si mtovu, kwalo sijitie pengo,  
 Changa hugeuka pevu, tizama embe na tongo,  
 Kipitacho kipe chongo, kitendo hakina kovu.

Ungalionia ni kovu, la kuumiza mgongo,  
 Ufanye jepe la povu, lifukie na udongo,  
 Moto mwishowe ni jivu, lakini si kiungo,  
 Kipitacho kipe chongo, kitendo hakina kovu.

Mngapi yalo matevu, kwa mataao na maringo,  
 Yatia kichevuchevu, ukachafuka ubongo,  
 Yakeshia upotevu, ja pepe ndani ya lingo,  
 Kipitacho kipe chongo, kitendo hakina kovu.

Twaa mfano wa ndevu, zimeoza hata shingo,  
 Zinazunguka mashavu, kusongana miringo,  
 Hazilemei kichevu, hazikutii kibyongo,  
 Kipitacho kipe chongo, kitendo hakina kovu.

Vyambiwa mvumilivu, msubiri japo bungo,  
 Hupata lililo bivu, bivu lisilo na chongo,  
 Bora kuwa mtulivu, mwaka huanza mwingo,  
 Kipitacho kipe chongo, kitendo hakina kovu.

### **Maswali**

- |  |           |
|--|-----------|
| (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka.                                   | (alama 1) |
| (b) Eleza sifa za shairi hili.   | (alama 5) |
| (c) Shairi hili linaweza kuwekwa katika bahari tofauti tofauti. Eleza. | (alama 3) |
| (d) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari.                         | (alama 4) |

- (e) Kwa kutoa mifano miwili, jadili idhini ya mwandishi wa shairi. (alama 4)
- (f) Eleza maana ya msamiazi ufuatao kama ulivyonumika katika shairi. (alama3)
- (i) Bungo
  - (ii) Twaa
  - (iii) Moyo kumpa kisongo

For More Free KCSE Past Papers Visit [www.FreeKCSEpastpapers.com](http://www.FreeKCSEpastpapers.com)